# Jarida la SIKONGE DC

Toleo No. 2 La Mwaka 2022









# YALIYOMO


3 RAIS SAMIA AFUNGUA BARABARA YA TABORA-KOGA-MPANDA(KM 342.9)

4 RC TABORA ASISITIZA KUONGEZA KASI UTEKELEZAJI WA ANWANI ZA MAKAZI.

5 RC TABORA AKAGUA MAJENGO SITA HOSPITALI YA WILAYA YA SIKONGE

6 WANAOHARIBU MIUNDOMBINU YA BARABARA KUCHULIWA HATUA.

7 UKUSANYAJI WA MAPATO KWA NJIA Y A KIELEKTRONIKI WASISITIZWA-SIKONGE.

8 MHE.KAKUNDA AMSHUKURU RAIS KWA KUONGEZA BAJETI YA TARURA-SIKONGE

22 NUKUU ZA VIONGOZI

23 KATUNI NA VIBONZO

# RAIS SAMIA AFUNGUA BARABARA YA TABORA-KOGA-MPANDA(KM 342.9)

ANa.Anna Kapama
18.5.2022

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan amefungua Barabara yaTabora-Koga-Mpanda yenye urefu wa Kilomita 342.9 inayounganisha Mkoa wa Tabora na Katavi na Kuzungumza na wananchi wa Sikonge.



*"Niombe sana Ndugu zangu kutunza miundombinu kwa manufaa yenu wenyewe, mnapoharibu mnajiharibia wenyewe..lakini pia wananchi toeni taarifa ili washughulikiwe wanaofanya uhalifu" Mhe.Samia Suluhu Hassan.*

Rais Samia amewasisitiza wananchi kutunza miundombinu ya Barabara kwa kuwa Serikali inatumia gharama kubwa kwa manufaa ya wananchi huku akiagiza Jeshi la Polisi kuwawajibisha wote watakaobainika kuharibu miundombinu hiyo.

"Niombe sana Ndugu zangu kutunza miundombinu kwa manufaa yenu wenyewe, mnapoharibu mnajiharibia wenyewe..lakini pia wananchi toeni taarifa ili washughulikiwe wanaofanya uhalifu" Mhe.Samia Suluhu Hassan.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa Barabara hiyo, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe.Prof.Makame Mbarawa amesema Barabara hiyo imegharimu Tsh. Bilioni 473.879 huku akitaja manufaa ya Barabara hiyo kuwa ni pamoja na kuleta manufaa kwa Mikoa husika kwani kutaimarisha Biashara katika Mkoa wa Tabora na Katavi, kiunganishi kikuu Cha bandari ya Dar es salaam na Nchi jirani ya Kongo,,kurahisisha uendeshaji wa Shughuli za kiuchumi ikiwemo Biashara na Kilimo sambamba na kuimarisha Uhusiano wa Kiuchumi na Mataifa jirani . Barabara hiyo ya Tabora-Koga-Mpanda imejengwa na Serikali ikishirikiana na Benki ya Maendeleo Afrika (AFDB) na imekamilika kwa asilimia 100%.



Kwa Upande wao wananchi wa Wilaya ya Sikonge wameipongeza Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe.Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza kwa vitendo miradi ambayo ina tija kwa wananchi.

# RC TABORA ASISITIZA KUONGEZA KASI UTEKELEZAJI WA ANWANI ZA MAKAZI.

Na.Anna Kapama



Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Balozi.Dkt.Batilda Buriani akiongea na Viongozi mbalimbali na waratibu wa anwani za makazi na kuwasisitiza kuongeza Kasi katika utekelezaji wa zoezi hilo alipokutana nao mapema leo.

"Tuko na Kamati ya Usalama ya Wilaya, ni dhahiri kabisa mnaendesha zoezi hili kama operesheni, muendeshe ki Oparesheni na nashukuru kwamba taarifa ziemeendelea kuingizwa.."RC Batilda

Aidha,amewahimiza kuwa wabunifu huku wakizingatia matumizi sahihi ya fedha yanayoendana na Viwango vya kazi.

"Lakini pia tuangalie gharama zinazotumika..tutakuwa ni Mkoa ambao tumekamilisha sio tu kwa kushinda lakini pia tutaangalia gharama tutakayokuwa tumeitumia na Viwango vile vya kazi." Balozi RC Balozi Batilda.




*"Tuko na Kamati ya Usalama ya Wilaya, ni dhahiri kabisa mnaendesha zoezi hili kama oparesheni, muendeshe ki Oparesheni na nashukuru kwamba taarifa ziemeendelea kuingizwa.."RC Batilda*

# RC TABORA AKAGUA MAJENGO SITA HOSPITALI YA WILAYA YA SIKONGE

Na Anna Kapama
21.4.2022





Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe.Balozi. Dkt Batilda Buriani akikagua majengo 6 ya Hospitali ya Wilaya ya Sikonge ambayo yamegharimu Tsh. Bilioni 1.1 ikiwa ni Fedha kutoka Serikali kuu za bajeti ya Mwaka 2021/2022 sambamba na Fedha za UVIKO-19.

Balozi Batilda amewaagiza wasimamizi wa majengo hayo kuongeza Kasi ili yakamilike kwa wakati uliopangwa yakiwa katika ubora unaotakiwa.

Majengo hayo ni pamoja na jengo la kuhifadhia Maiti (Mochwari) jengo la wodi ya upasuaji ya wanaume na Wanawake, Jengo la kuwahudumia wagonjwa wa dharura (EMD), Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi, pamoja na Jengo la upasuaji.

Aidha, jitihada hizi zinafanywa na Serikali kwa lengo la kusogeza huduma za Afya karibu na jamii ili kupunguza vifo visivyo vya lazima kwa wananchi ili kujenga jamii yenye Afya Bora.

# WANAOHARIBU MIUNDOMBINU YA BARABARA KUCHULIWA HATUA.


Na Anna Kapama
21.4.2022



Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe.Dkt.Balozi Batilda Buriani akikagua Kipande Cha Barabara kinachojengwa kwa kiwango cha lami chenye urefu kwa Mita 400 kutoka Barabara kuu kwenda Ikulu ndogo ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge kitakachogharimu Tsh. Milioni 185.5 .

Balozi Batilda amempongeza Meneja wa TARURA Wilaya ya Sikonge Mhandisi Eligdius Method kwa kusimamia vyema kwa Viwango huku akitoa rai kwa wananchi wanaoharibu miundombinu ya Barabara inayojengwa kwa gharama kubwa kuacha maramoja.

Aidha,Balozi Batilda amemuagiza Mkuu wa Wilaya ya Sikonge kuchukua hatua Kali kwa watakaobainika kuharibu miundombinu hiyo ikiwemo taa za Barabarani..



# UKUSANYAJI WA MAPATO KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI WASISITIZWA-SIKONGE.

Na.Anna Kapama.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Mhe.Rashid Magope amesisitiza Ofisi ya Mkurugenzi kusimamia ukusanyaji wa Mapato hasa kwa kutumia mashine za kielektroniki na kwa uaminifu ili Mapato yaweze kuongezeka zaidi ya ilivyo sasa ili Halmashauri iweze kutoa huduma Bora kwa wananchi.

Mhe.Magope ameyasema hayo alipofungua Mkutano wa Baraza la Madiwani na kuongeza kuwa Mapato ya ndani ni muhimu kwa kuwa yanasaidia kuendesha shughuli za Halmashauri ikiwemo kutoa huduma za kijamii kwa wananchi. "Niwaombe Mkurugenzi na wataalamu kujipanga kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha Mapato yanaongezeka, bila Mapato ya ndani hatuwezi kutoa huduma stahiki kwa wananchi"Mhe.Magope.

Akitoa Salamu kwa madiwani na wananchi waliohudhuria baraza hilo, mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Faraja Hebel amewasisitiza wananchi kutoa ushirikiano katika zoezi la usajili wa anwani za makazi akizitaja baadhi ya faida za kuwa na anwani za makazi.

"Lengo la Serikali ni kuhakikisha kila mwananchi anapata anwani yake ya makazi na anwani hiyo itarahisisha huduma za posta, pamoja na utoaji wa huduma hasa majanga yanapotokea, pamoja utumaji wa mizigo na vifurishi, ...zoezi hili linatakiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Aprili, 2022."

Katika baraza hilo baadhi ya madiwani wameuliza maswali ya papo kwa papo kwa Mkurugenzi juu ya uboreshaji wa miundombinu hasa ya Barabara katika Kata za Mole, Kisanga na Kirumbi maswali ambayo yalielekezwa kwa Meneja wa TARURA Wilaya na kutolewa ufafanuzi kwamba Serikali imeendelea kutoa fedha kwa awamu katika ukarabati na ujenzi wa Barabara na kuongeza kuwa Barabara hizo ziko ndani ya mpango wa kuboreshwa huku akitaja kuwa tayari fedha zimeshatolewa kwa baadhi ya Barabara ikiwemo Barabara ya Makibo-Nyahua Tsh.Milioni 190 zimetolewa kwa ajili ya ukarabati huo.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imepanga kukusanya Tsh.Bilioni 3.2 ya Mapato ya ndani fedha ambazo zitasaidia kutoa huduma kwa jamii ikiwemo kutoa asilimia 10% ya Mapato hayo kwa ajili ya Vikundi wanawake,vijana na watu na wenye ulemavu ili waweze kujikwamua kiuchumi.



# MHE.KAKUNDA AMSHUKURU RAIS KWA KUONGEZA BAJETI YA TARURA-SIKONGE



18.5.2022

Mbunge wa Jimbo la Sikonge(CCM) Mhe. Joseph Kakunda amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ya Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Sikonge kwa asilimia 193 kutoka TSH.Milioni 820 hadi Bilioni 4.19 fedha ambazo zitasaidia kujenga na kuboresha miundombinu ya Barabara za Mjini na Wilayani hapo



# DC PALINGO AZINDUA MPANGO WA KUSAJILI NA KUTOA VYETI VYA KUZALIWA KWA WATOTO WA UMRI CHINI YA MIAKA MITANO-SIKONGE.

**UZINDUZI WA MPANGO WA KUSAJIRI WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Mkuu Wa Wilaya Ya Sikonge Mhe. John Palingo.ambae ni Mgeni Rasmi akiwakabidhi wazazi vyeti vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Na.Anna Kapama.
3.6.2022

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe.John Palingo amezindua Mpango wa Kusajili na Kutoa Vyeti vya kuzaliwa kwa Watoto wenye Umri Chini ya Miaka Mitano Wilaya ya Sikonge na kuwataka Wananchi kutumia fursa hiyo kuwaleta watoto wasajiliwe na kupata vyeti vya kuzaliwa. DC Palingo amesema mpango huo ni muhimu hivyo kila Mwananchi Mwenye mtoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano ana haki ya kusajiliwa na kupata Cheti Cha kuzaliwa Bure.

“Naishukuru Serikali kwa Kuleta Mpango huu katika eneo letu na pia naipongeza RITA kwa juhudi inazofanya katika kuleta mabadiliko chanya katika masuala ya Usajili” DC PALINGO.

Aidha, DC Palingo amewataka Wasajili Wasaidizi kutotumia mpango huo kama fursa ya kujipatia kipato . “Natoa maelekezo kwamba yeyote atakaekiuka Misingi ya utendaji ya mpango huu kwa makusudi hatua zichukuliwe kwa mujibu wa Sheria” amefafanua.

Kwa Upande wake Mratibu wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano Cloud Nkanwa amesema Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inategemea Kusajili watoto 44,047 walio na Umri Chini ya Miaka Mitano na hawana vyeti vya kuzaliwa kwa muda wa wiki mbili na kuongeza kuwa mfumo huo utaendelea kuwepo ili kuweza kuwasajili na kuwapatia vyeti Watoto watakaozaliwa .

# WILAYA YA SIKONGE YAADHIMISHA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI KWA KUPANDA MITI.

Na.Anna Kapama
Tarehe 5.6.2022

Ikiwa ni Siku ya Mazingira Duniani Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imeadhimisha siku hiyo kwa kupanda Miti katika maeneo mbalimbali ikiwemo Kata ya Pangale, ambapo Viongozi mbalimbali wamehudhuria akiwemo Kaimu Katibu Tawala Wilaya ya Sikonge Faraja Hebel, Wakala wa Misitu(TFS) Wilaya ya Sikonge, na wataalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi.

Kaimu Katibu Tawala Faraja Hebel amewasisitiza wananchi kutunza Mazingira kwa kupanda Miti pamoja na kutunza vyanzo vya Maji kwa kuwa ni muhimu kwa maisha ya wanadamu na viumbe hai.

Aidha, Hebel amewaasa wananchi kutokufanya Shughuli za kibinadamu kwenye Vyanzo vya Maji akiwataka kuwa mabalozi wazuri katika kutunza vyanzo hivyo kwa kupanda Miti.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, Afisa Mazingira Wilaya ya Sikonge Bwenge Antidius ametoa Elimu ya upandaji Miti na namna ya kuitunza na kuongeza kuwa upandaji na utunzaji wa Miti unapaswa kuwa endelevu na siyo siku maalumu.

Katika kuunga mkono juhudi za kuhifadhi Mazingira Ofisi ya Wakala wa huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Sikonge imetoa Miche 483 ambayo imepandwa na Viongozi pamoja na wananchi katika maeneo yao.





# MIRADI MIWILI YA MAJI YAZINDULIWA SIKONGE



Na Anna Kapama

Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mhe.Dkt. Yahaya Nawanda amemuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe.Balozi.Dkt.Batilda Buriani katika uzinduzi wa Miradi ya Maji katika Vijiji vya Utimule na Msuva na kuwataka Wananchi kutunza miundombinu ya Maji ili wanaufaike kwa muda mrefu.

Akizungumza na Wananchi wakati wa uzinduzi Mhe.Nawanda amesema Serikali imedhamiria kutoa huduma zote stahiki kwa wananchi ikiwemo huduma ya Maji kwa lengo la kumtua mama ndoo.

Akisoma taarifa ya miradi hiyo Meneja wa RUWASA Mhandisi Fikiri Samadi amesema Miradi yote miwili imegharimu Tsh.Milioni 319.2 kwa Vijiji vya Msuva na Utimule na inahudumia jumla ya watu 2350 Kijiji Cha Msuva na watu 1869 kijijini Utimule.



Kwa Upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Mhe.Rashid Magope ameipongeza Serikali kwa kuendelea kutimiza ahadi za utekelezaji wa Miradi mbalimbali ikiwemo ya Maji katika Wilaya ya Sikonge.

Uzinduzi wa Miradi hiyo ya Maji umewapunguzia adha wananchi ambao walikuwa wakitembea umbali mrefu kufata Maji ambapo walikuwa wanatumia muda mrefu na sasa Maji yanapatikana karibu katika maeneo yao.

# TSH.MILIONI 412.4 ZA TASAF KUNUFAISHA ZAIDI YA KAYA 5000- SIKONGE

Na Anna Kapama

Serikali kupitia Mpango wa kunusuru kaya Masikini (TASAF) imetoa fedha ikiwa ni awamu ya tatu fedha ambazo zimeanza kutolewa kwa kaya Masikini kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi. Mratibu wa TASAF Wilaya ya Sikonge Cloud Nkanwa amesema Tsh.Milioni 412.4 zinalenga kunufaisha kaya 5758 katika vijiji 64 vinavyopatika katika Wilaya hiyo huku akiwataka wanufaika wa mpango huo kuzitumia fedha hizo katika mambo yenye tija.

"Lengo la mpango huu ni kuinua hali ya maisha na kuongeza kipato, kuwajengea uwezo na kunusuru kaya Masikini zilizo katika Mazingira hatarishi, jambo ambalo Serikalini imekuwa ikilifanya kwa wananchi" Mratibu wa TASAF. Katika hatua nyingine wananchi ambao ni wanufaika wa TASAF wameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwapatia fedha ambazo zimewasadia katika kutatua changamoto mbalimbali .



"Fedha za TASAF zimenisaidia kufanya Biashara ndogondogo, pamoja na kufuga kuku, na kupitia Biashara nimejenga nyumba ya Bati ambayo mwanzo sikuwa nayo" Mnufaika wa TASAF. Fedha hizo zinalenga kuwawezesha kupata mahitaji ya Msingi na fursa za kujijiongezea kipato kwa njia ya uzalishaji Mali kupitia fedha hizo kwa ajili ya manufaa ya muda mrefu.



# TSH.MILIONI 470 KUJENGA MIUNDOMBINU SHULE YA SEKONDARI NYAHUA.

Anna Kapama
29, Machi 2022



Serikali ya awamu ya Sita kupitia Programu ya kukuza ubora wa Elimu ya Sekondari(SEQUIP) imetoa Tsh.Milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ikiwemo vyumba 8 vya Madarasa , Matundu 20 ya Vyoo, Maabara 3, Jengo la Utawala na Chumba kimoja Cha Kopyuta. Aidha, ujenzi huo unaotarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi May, 2022 utaipelekea Shule hiyo kutoka Shule ya Sekondari Shikizi na Kuwa Shule ya Kata ambapo itawarahisishia wanafunzi wa kidato cha Nne waliokuwa wakienda kufanya mitihani ya Taifa katika Shule ya Sekondari Igigwa



*"Ongezeni Juhudi mmalize kwa wakati na ubora unaotakiwa kulingana na mikataba iliyowekwa"DC Palingo.*



# KAMATI YA SIASA MKOA WAPONGEZA MIRADI INAYOTEKELEZWA WILAYANI

Anna Kapama
Machi 20, 2022.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa Kamati ya Siasa Mkoa wa Tabora imefanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya maendeleo inayotekelezwa Wilaya ya Sikonge na kuwapongeza kwa ujenzi wa Viwango vinavyotakiwa pamoja na usimamizi mzuri ya miradi hiyo. wa Tabora Hassan Wakasuvi amesema lengo la ziara hiyo ni kuhakikisha inasimamia fedha zinazoletwa na Serikali kwa ajili ya miradi ya Maendeleo zinakamilika kwa wakati na kwa Viwango ili zilete tija kwa wananchi. Kamati hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora Hassan Wakasuvi imekagua ujenzi wa Vyumba 3 vya madarasa ya UVIKO-19 uliogharimu Tsh.Milioni 60 katika Shule ya Sekondari Kamagi na kuwapongeza kwa kuwa tayari yanatumika vyema.

Aidha, Kamati hiyo imekagua mradi wa ujenzi wa wodi ya wazazi Kituo Cha Afya Tutuo uliogharimu Tsh.Milioni 250, ikiwa ni fedha za tozo za miamala ya Simu mradi ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo Machi 25,2022. Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe.John Palingo ameipongeza Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe.Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha nyingi za miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Mwaka mmoja wa Uongozi wake katika Sekta mbalimbali ikiwemo Afya,Elimu,Maji na Miundombinu ya Barabara .



# RAS TABORA AKAGUA MIRADI YA AFYA-SIKONGE.

Anna Kapama

Katibu Tawala Mkoa wa Tabora Mhe.Msalika Makungu amefanya ziara Wilayani Sikonge na kukagua Hospitali teule ya Wilaya ya Sikonge , Zahanati ya Sikonge pamoja na ujenzi wa Jengo la Huduma za dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya. RAS ambae aliambatana na wataalamu mbalimbali wameipongeza Hospitali pamoja na Zahanati kwa kuboresha Mazingira ambayo ni rafiki kwa wagonjwa kupata huduma. Aidha, amewasisiza kuendelea kuboresha miundombinu ya Afya hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali ya awamu ya Sita inatoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Afya,na kuongeza kuwa Wilaya ya Sikonge ni lango la kuingilia kwa kuwa ni njia inayopitia bandari ya Kalema Mkoani Katavi kuelekea Nchini Congo.

“Tarajieni kupokea wageni wengi kutoka nchi za kusini kwa kuwa magari ya mizigo yatapita hapahapa Sikonge kuelekea bandari ya Kalema ambayo itakamilika mwezi wa Sita ambayo ndio inasafirisha bidhaa kwenda Congo.. watahitaji huduma mbalimbali zikiwemo za Afya,,,hivyo mjipange kuboresha zaidi miundombinu ya Afya kwa kuwa mtakuwa na wageni wengi zaidi kutoka nje”RAS Msalika. Kwa upande wake Mratibu kutoka Mfuko wa Malipo kwa Ufanisi(RBF) Tausi Yunge ameipongeza Zahanati ya Sikonge ambayo ilipokea Tsh.Milioni 34.6 kutoka “RBF” kwa ajili ya ujenzi wa miondombinu mbalimbali kwa kuwa na Mazingira safi nje na ndani pamoja na mpangilio mzuri wa taarifa mbalimbali za wagonjwa. Naye,Mhasibu kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Simon Mality amewasisitiza watumishi wa

Afya kutumia mfumo wa kielektroniki wa kukusanya taarifa za wagonjwa pamoja kutunza kumbukumbu( GoT_HoMIs) kwa kuwa unarahisisha utoaji huduma kwa wagonjwa pamoja na kukusanya Mapato kwa Ufanisi. Aidha, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Sikonge Seleman Pandawe ameahidi kutekeleza maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na Katibu tawala.



*“Tarajieni kupokea wageni wengi kutoka nchi za kusini kwa kuwa magari ya mizigo yatapita hapahapa Sikonge kuelekea bandari ya Kalema ambayo itakamilika mwezi wa Sita ambayo ndio inasafirisha bidhaa kwenda Congo..watahitaji huduma mbalimbali zikiwemo za Afya,,,hivyo mjipange kuboresha zaidi miundombinu ya Afya kwa kuwa mtakuwa na wageni wengi zaidi kutoka nje”RAS Msalika.*

# VIJANA 100 KUNUFAIKA NA MAFUNZO YA KITALU NYUMBA-SIKONGE.

Anna Kapama.

Mafunzo ya kitalu nyumba(Greenhouse) yamefunguliwa rasmi leo Wilayani Sikonge na Wataalamu wa masuala ya Kilimo kutoka Chuo kikuu Cha Kilimo Sokoine (SUA) ikiwa ni juhudi za Serikali kuwakwamua wananchi kwa kuwapatia Elimu ya Kilimo chenye tija. Aidha Mratibu wa Mradi huo Huseni Mchomvu amesema lengo la mradi huo ni kuwapa uelewa na kuwasaidia vijana






kutambua Kilimo Biashara chenye tija ili hata Mikopo ya asilimia 6% kati ya 10% inayotolewa na Halmashauri kwa makundi ya Vijana na watu wenye Ulemavu iweze kuwanufaisha kupitia Kilimo hicho. Mafunzo hayo ambayo yatadumu kwa takribani siku 14 yamedhaminiwa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge , Kazi, Vijana,ajira na wenye Ulemavu.



# DC PALINGO ASISITIZA UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA ANWANI ZA MAKAZI

Anna Kapama.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe.John Palingo amefanya ziara Tarafa ya Kiwere na kufuatilia mwenendo wa zoezi la anwani za makazi na kuzungumza na Viongozi wa Tarafa hiyo wakiwemo watendaji wa Kata na Vijiji ambao wanasimamia kwa karibu kwa ngazi ya Kata. Aidha, DC Palingo amewapongeza Viongozi wa Tarafa ya Kiwere kwa kukamilisha utekelezaji wa anwani za makazi na kuwahimiza wale ambao bado hasa kwa Tarafa ya Sikonge kumaliza kwa wakati ili ifikapo Aprili 25, 2022 zoezi liwe limekamilika. DC Palingo amewasisitiza wananchi kutoa ushirikiano katika maeneo ambayo bado zoezi hilo linaendelea. Utekelezaji wa zoezi la anwani za makazi Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge umefikia kaya 44,148 sawa na asilimia 90.4% ya kaya 48,835 zinazokadiriwa kusajiliwa. Katika hatua nyingine DC Palingo amekagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika Tarafa hiyo ikiwemo Shule Shikizi ya Muwale, Shule ya Sekondari Kipili, pamoja ujenzi wa Matundu matano ya Vyoo katika Kituo Cha Afya Kitunda.
Aidha, amewasisitiza kukamilisha kwa wakati ili wananchi wa maeneo hayo wapate huduma stahiki na kwa wakati huku akitahadharisha matumizi ya fedha yaendane na thamani ya miradi hiyo.





# YANAYOAGIZWA NA WAJUMBE WA KAMATI YAZINGATIWE" MHE.MAGOPE

Na Anna Kapama
21.4.2022

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Mhe.Rashid Magope amewasisitiza wataalamu wa Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo kutekeleza maagizo yanayotolewa na Viongozi mbalimbali wanapopita kukagua . Mhe.Magope ameyasema hayo wakati Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ikifanya ziara katika Kata ya Nyahua na kukagua miradi ya Maendeleo ikiwemo Shule ya Sekondari Nyahua na kuongeza kuwa mapungufu yanayotolewa na Viongozi wanapopita kukagua yanaimarisha utendaji wao na hatimaye kujenga miradi iliyo na Ubora..

Kamati hiyo ya Fedha Uongozi na Mipango imekagua ujenzi wa miundombinu ikiwemo vyumba 8 vya Madarasa , Matundu 20 ya Vyoo, Maabara 3, Jengo la Utawala na Chumba kimoja Cha Kopyuta mradi wenye thamani ya Tsh.Milioni 470 kutoka Serikali ya awamu ya Sita kupitia Programu ya kukuza ubora wa elimu ya Sekondari(SEQUIP) sambamba na kukagua mradi wa Ujenzi wa Matundu matatu ya Vyoo katika Zahanati Nyahua.



Balozi Batilda amewaagiza wasimamizi wa majengo hayo kuongeza Kasi ili yakamilike kwa wakati uliopangwa yakiwa katika ubora unaotakiwa. Majengo hayo ni pamoja na jengo la kuhifadhia Maiti (Mochwari) jengo la wodi ya upasuaji ya wanaume na Wanawake, Jengo la kuwahudumia wagonjwa wa dharura (EMD), Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi, pamoja na Jengo la upasuaji (Theatre). Aidha, jitihada hizi zinafanywa na Serikali kwa lengo la kusogeza huduma za Afya karibu na jamii ili kupunguza vifo visivyo vya lazima kwa wananchi na kujenga jamii yenye Afya Bora.



# MAOMBI YA NAFASI ZA KAZI YA SENSA NI BURE.






Kamisaa wa Sensa ya watu na Makazi Mhe.Anne Makinda amesema maombi ya nafasi za kazi ya SENSA ya watu na Makazi ni bure ikiwemo huduma ya ugongaji wa muhuri kutoka kwa Maafisa watendaji wa Kata na Vijiji .

Mhe.Makinda ameyasema hayo leo Mei 12, 2022 wakati akizungumza na Maafisa Habari na Uhusiano wa Serikali juu ya maandalizi ya Sensa ya watu na Makazi na wajibu wao katika kufanikisha zoezi hilo kwenye kikao kazi Cha 17 Cha Maafisa hao kinachoendelea Jijini Tanga.

Aidha, amewasisitiza Maafisa Habari na Uhusiano wa Serikali kushiriki kikamilifu katika utoaji wa Elimu na Hamasa kuhusu SENSA kwa wananchi ili waweze kushiriki zoezi hilo muhimu kwa maendeleo ya wananchi na Taifa.

Amewashauri watendaji wa Kata na Vijiji kutokuomba kazi hiyo kwa kuwa wao ni waratibu wa zoezi hilo katika maeneo yao.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan amefungua Barabara yaTabora-Koga-Mpanda yenye urefu wa Kilomita 342.9 inayounganisha Mkoa wa Tabora na Katavi*



*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge (wa Nne kutoka kulia) katika Picha ya pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri hiyo.*



*Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Sikonge Mhe.Anna Chambala akizungumza na Wananchi wa Kata ya Tutuo wakati wa Kamati ya Siasa Mkoa ilipotembelea na kukagua miradi ya Maendeleo*



*Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe. John Palingo ametembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Shule ya Sekondari Shikizi Nyahua Kata ya Nyahua na kuwasisitiza kujenga kwa Ubora na kwa wakati.*




***Katibu Tawala Mkoa wa Tabora Mhe.Msalika Makungu akifanya ziara Wilayani Sikonge na kukagua Hospitali teule ya Wilaya ya Sikonge , Zahanati ya Sikonge pamoja na ujenzi wa Jengo la Huduma za dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya.***




***Mafunzo ya kitalu nyumba(Greenhouse) yamefunguliwa rasmi Wilayani Sikonge na Wataalamu wa masuala ya Kilimo kutoka Chuo kikuu Cha Kilimo Sokoine (SUA) ikiwa ni juhudi za Serikali kuwakwamua wananchi kwa kuwapatia Elimu ya Kilimo chenye tija.***




***Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Mhe.Rashid Magope akiwasisitiza wataalamu wa Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo kutekeleza maagizo yanayotolewa na Viongozi mbalimbali wanapopita kukagua .***

# "NUKUU ZA VIONGOZI


*"Kuna wafugaji wengi wa nyuki, wazalishaji wa asali.. nimefurahi sana Kusikia kwamba Benki ya Maendeleo Afrika (AFDB) wametoa fedha kwa ajili kuwafundisha wafugaji wa Nyuki Sikonge na TFS imejenga kiwanda Cha Asali Sikonge,hakikisheni asali inazalishwa kwa Viwango vya kimataifa.."Mhe Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipozungumza na wananchi Wilaya ya Sikonge.*






*"Kazi hiyo uliyonayo ukiifanya kwa upendo,Moyo wako utakuwa na Furaha, lakini ukiifanya kwa manung'uniko utakuwa mtumwa wa kazi hiyo" Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Ndg.Seleman Pandawe alipokuwa akizungumza na watumishi wa Halmashauri hiyo tarehe 23.5.2022.*


# KATUNI NA VIBONZO









**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE.**



**S.L.P 70,SIKONGE.**
**Simu: +255262965732**
**Barua pepe. ded@sikONGE.go.tz**
**Tovuti. www.sikongedc.go.tz**
**Instagram. @sikongedc**
**Facebook.@sikongedc**